

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

Simu Na. 026-2702647
Fax Na. 026-2702202



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa
S.L.P 162,
IRINGA.

TANGAZO LA NAFASI ZA VYUMBA VYA BIASHARA KATIKA STENDI YA
IGUMBILO.

Mkurugenzi wa manispaa ya Iringa anapenda kuwatangazia wananchi wote wanaohitaji vyumba vya biashara katika jengo la abiria lililopo katika stendi ya Igumbilo kuwasilisha maombi kwa utaratibu ufuatao:

1. Waombaji wenye nia na uwezo wa kupangisha vyumba wanaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kusoma kabrasha lenye fomu ya maombi pamoja na rasimu ya mkataba katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa Iringa kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi 9.30 jioni siku ya Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa kwa siku za sikukuu. Fomu za maombi zitaanza kutolewa tarehe 15/03/2022
2. Stendi ya kisasa ya Igumbilo inakusudiwa kutoa huduma za aina mbalimbali kwa wateja wake hivyo mwombaji atatakiwa kuleta maombi ya chumba cha biashara na kuainisha aina ya biashara katika chumba anachoomba katika fomu ya maombi.
3. Kodi ya pango italipwa kwa mujibu na utaratibu utakaotolewa na Halmashauri ya Manispaa kwa wale wote watakaofanikiwa kupata vyumba vya biashara katika Stendi ya Igumbilo kwa mchanganuo ulioanishwa katika fomu ya maombi.
4. Gharama za bili za matumizi ya umeme na maji litakuwa ni jukumu la mpangaji atakayefanikiwa kupata cumba cha biashara.

5. Mwombaji atakayepata chumba cha biashara na kuingia mkataba na Halmashauri atatakiwa kulipa kodi ya pango kwa mkupuo wa mwaka au miezi sita. Aidha ambae hatafanya biashara katika fremu yake kwa muda unaozidi miezi mitatu bila sababu ya msingi atanyang'anywa na kupewa mtu mwingine.
6. Idadi ya vyumba vya biashara ni vichache hivyo hakuna mwombaji atakayetakiwa kuomba chumba zaidi ya kimoja ili kutoa fursa sawa kwa waombaji wengine. Aidha mwombaji atakayefanikiwa kupata fremu na kuingia Mkataba na Halmashauri **hataruhusiwa kumpangisha mtu mwingine.**
7. Mwombaji anasisitizwa sana kutembelea eneo la Stendi na kukagua kabla hajaainisha katika maombi yake aina na namba ya chumba anachoomba. Idadi ya vyumba ni vichache hivyo kufanikiwa au kutofanikiwa kwa maombi ya mwombaji kutategemea kuwahi kuchukua form na kulipia kwa wakati.
8. Maombi yote yafungwe katika bahasha na kuandikwa **“MAOMBI YA UPANGAJI WA CHUMBA CHA BIASHARA NA”** na yatumwe kwa **Mkurugenzi wa Manispaa, SLP 162 IRINGA. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/03/2022 Saa 4.00 Asubuhi**

Limetolewa na:-

MKURUGENZI WA MANISPAA IRINGA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

Simu Na. 026-2702647
Fax Na. 026-2702202



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa
S.L.P 162,
IRINGA.

**FOMU YA MAOMBI YA VYUMBA VYA BIASHARA/VIZIMBA/MGAHAWA KATIKA STENDI YA
IGUMBILO**

1. Majina ya Mwombaji.....
2. Anwani ya Posta ya Mwombaji.....
3. Namba ya Simu ya Mwombaji.....
4. Mtaa.....Kijiji.....Kata.....Wilaya.....
5. Aina ya kibanda Mwombaji anachoomba
.....
6. Namba ya Stakabadhi ya malipo
.....
7. Mwombaji aambatanishe ushahidi wa chanzo cha mapato kwa ajili ya biashara kama vile kuwa na mshahara, biashara na kilimo au kuwa na uhakika wa kupata fedha toka taasisi za fedha au watu binafsi.....
8. Aina ya biashara tarajiwa ya
Mwombaji.....
9. Kwa Mwombaji atakayepewa chumba atatakiwa kulipa kodi ya pango ya Tshs.....kwa mwezi, kwa muda wa miezi sita au mwaka mzima
10. Nathibitisha kuwa nitatimiza masharti yote ya upangaji kama yaliyovyoainishwa kwenye kielelezo cha mkataba kilichoambatishwa iwapo nitafanikiwa kupata nafasi ya kufanya biashara.